

# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI**

Shule ya Sekondari Rusimbi,  
S. L. P 479,  
**KIGOMA.**

14/12/2021.

**KUMB. NA.....**

**Mwanafunzi: .....**

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2021.**

**1.0.** Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **04/01/2021** ili kufanya maandalizi ya kozi ya kiingereza. Tarehe ya mwisho wa kuripoti ni tarehe **01/02/2021**.

### **2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

#### **2.1 SARE YA SHULE**

##### **(a) WAVULANA**

1. Shati nyeupe mbili mikono mifupi
2. Suruali rangi ya light blue(Kitambaa kimeambatanishwa).
3. Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi (ngozi)
4. Jozi za soksi nyeupe ndefu mbili (2) na mkanda mweusi
5. Sare za michezo Bukta nyeusi na Tisheti ya bluu.

##### **(b) WASICHANA**

1. Shati vyeupe mbili mikono mifupi
2. Sketi rangi ya kijani (mshono ataelekezwa)
3. viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi (ngozi)
4. Soksi nyeupe ndefu pea mbili
5. Sare za michezo Bukta nyeusi na Tisheti ya bluu.

#### **2.2 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:**

**2.3** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa. Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara tu baada ya kuripoti shulenii:-

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kusoma/kujifunza kwa bidii na kufanya mazoezi/Majaribio yanayotolewa ndani na nje ya shule.
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilfu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g) Kuvala kwa unadhifu sare ya shule uwapo shulenii
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**2.4. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule:-**

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga.
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungu,kuberi n.k.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani au nje ya shule au kutia mimba.
10. Kutoa mimba
11. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shulenii.

**2.5. MAMBO MENGINE MUHIMU:**

- (a). Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shulenii.
  - (b) Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi
  - (c) Fomu ya mzazi kukiri/kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa Ada,Michango na maelekezo mengine yatatolewa na Mkuu wa Shule.
  - (d) Cheti cha kuzaliwa.
- 2.6. Tafadhalii soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



.....

**AYUBU MGANDE  
MKUU WA SHULE**

HEADMASTER  
RUSIMBI SEC. SCHOOL  
P.O. Box 476  
GOMA